

DHORUBA IJAYO



Na tuendelee kusimama kwa muda kidogo tu, kwa ajili ya maombi. Na tuinamishe vichwa vyetu.

Baba yetu wa Mbinguni mwenye Neema, kweli sisi ni watu walio na majaliwa, usiku wa leo, kwamba tunaweza kuangalia uso Wako wenye utukufu na kukuita Baba yetu; tukijua kwamba tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani, kwa sababu kwamba Roho Mtakatifu anashuhudia pamoja nasi, kwamba sisi ni wana na binti za Mungu. Na Yeye ndiye shahidi wetu, kwamba tumeupita mstari huo; kwa kuwa mambo ya ulimwengu, ambayo tulikuwa tukiyapenda na kuyafurahia sana, yamekufa sasa. Nasi tumeinuliwa upya, pamoja na Kristo, na kuketi pamoja katika ulimwengu wa Roho, katika Yeye, tukiufurahia Uwepo Wake. Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hili!

² Basi, usiku wa leo, kwenye hafla hii, tungeomba ya kwamba ungetutembelea kwa njia kuu, usiku wa leo. Bariki kanisa hili dogo, ambalo tunalipenda, na ushirika mkuu na upendo tulio nao kwake na mchungaji wake, na kwa washirika wote, na kwa wale wanaoshiriki pamoja nasi hapa katika mkutano huu.

³ Basi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba usiku wa leo utakuwa ni usiku maalum, ambao tutakumbuka kwa muda mrefu Uwepo Wake usiku wa leo.

⁴ Jalia, kama kuna wengine, usiku wa leo, hapa ambao hawamjui Bwana Yesu kama Mwokozi wao binafsi, jalia wampate usiku wa leo, Bwana, Yule ambaye ameenda nyikani kumtafuta kondoo aliyepotea ambaye hajarudi kwenye zizi. Tujalie, Bwana. Na jalia kuwe na rehema kambini, usiku wa leo, kwa kuwa hilo ndilo tunaloomba. Katika Jina la Bwana Yesu, tunaomba hili. Amina.

Mwaweza kuketi.

⁵ Ni vema sana kurudi kwenye maskani hii, ama kanisa, usiku wa leo, kuwa na ushirika mzuri. Na leo hii nimeishia tu vibamba vidogo kutoka kwenye ule mkutano wa jana jioni.

⁶ Na nikiangalia huko nje kwenye wasikilizaji, na kuwaona watu mbalimbali, na nyuso ambazo nimekutana nazo. Jinsi ambavyo mimi, nyakati zilizopita, nimetamani kuangalia huko nje na kupeana mikono nao, ama kitu fulani. Lakini, loo, tulikuwa tumechelewa kidogo, nami ilinibidi tu kuharakisha. Bali nawatakeni kujua ya kwamba kulikuwako na wengi hapa jana jioni, ambao niliwatambua kutoka kwenye mikutano mingine.

⁷ Na, sasa, jana usiku nilipoenda nyumbani nami nilikuwa nikimwambia mke wangu, nikasema, “Sijui itakuwaje

tutakapouvuka ule mstari?” Nikisimama kule, nikiangalia chini, na kusema, “Vema, yule pale Ndugu *Fulani-wa-fulani!* Na pale...” Loo, huo utakuwa ni wakati mzuri sana! Nasi tunaitazamia siku hiyo, na hivi karibuni, karibuni. Wala sijui itakuwa ni lini, bali bila shaka utakuwa ni wakati mtukufu sana. Ninaamini ya kwamba Yohana, akiisha kuuona ule utukufu mkuu wa Mungu, nao ulikuwa umefunuliwa kwake, katika *Ufunuo*, yeye alisema, “Hata hivyo, na uje, Bwana Yesu.” Aliona ya kwamba ulikuwa ni mzuri sana.

Machache, yapata majuma mawili yaliyopita, nilikuwa huko Kingston, Jamaica.

⁸ Ndipo watu wengi wakafikiri, na wangali wanafikiria bado, kwamba maono hutokea tu jukwaani. Jamani, hayo si hata moja katika kumi yake. Hayo si moja katika tisini yake. Yanatokea wakati wote, kila mahali, na hakuna hata wakati mmoja ambapo moja limekosea.

⁹ Nao Wafanyabiashara Wakristo, Wafanyabiashara wa Full Gospel, nilikuwa nikiwatembelea, ama kule kama mgeni wa hilo tawi. Na usiku wa siku mbili zilikuwa zimepita, nasi tulikuwa tumekuwa na kuhubiriwa kwa Injili; halafu basi, na kusudi kupata kufahamiana na kusanyiko na kuihisi roho ya watu. Basi nilisema, “Ninaamini ingetosha, usiku wa leo, kama tukisambaza kadi za maombi, na kuanza kuwaomba wagonjwa.” Naye Bwana alitubariki. Ndipo usiku wa pili ukapita.

¹⁰ Na halafu tulikuwa tumeingia katika chu—chumba cha kulia kwenye Hoteli ya Flamingo, ambako, “uga” tungekuita hapa, ambako tulikuwa tukikaa. Na kila kitu huko kimewekwa msingi katika mpangilio wa Kizungu; unapolipa kodi yako ya nyumba, unalipa bili yako ya chakula; yote yanaambatana na ko—kodi ya nyumba. Nasi tulikuwa tukila kiamshakinywa. Na kulikuwako na kundi kubwa la Wanaume wa Full Gospel kule, pamoja na wengine, pia. Ndipo swali likazuka, “Hayo maono,” walisema, “ni ya ajabu sana. Ingekuwa ni ajabu sana kama yangetokea kila mahali.”

¹¹ “Loo,” nikasema, “yanatokea, kweli kabisa.” Kisha nikasema, “Hayo hayamponyi mtu yeyote.” Nikasema, “Kama mlipata kuona, mimi huwauliza watu, ‘Hilo litaisaidia imani yako, kumwamini Mungu?’”

¹² Maono hayaponyi; Kristo amefanya hivyo tayari. Ni kuisaidia tu imani yako. Ni kitu fulani tu ambacho Mungu aliongezea; baraka aliyoahidi kutuma, thibitisho la siku za mwisho. Tutaliingilia hilo baadaye, kote kwenye hili juma.

¹³ Lakini tulikuwa tumeketi mezani, nami nikasema, “Hapa sasa, Roho Mtakatifu yuko sasa.” Naye Ndugu Shakarian, wengi wenu mnamjua, Ndugu Demos, na rafiki yangu wa karibu sana; na Ndugu Arganbright, na, loo, watu wengi sana mbalimbali,

Ndugu Sonmore, marais na makamu wa marais, na kadhalika, wa Wanaume wa Full Gospel.

¹⁴ Nami nikasema, “Mvulana huyu anayekuja hapa ni mgonjwa,” mhudumu. Ndipo akakaribia mezani, naye Roho Mtakatifu akaanza kumzungumzia, na kumwambia, kasema, “Sasa, unaugua ugonjwa wa moyo. Mke wako, pia, ni Mkristo. Unaamini, ila unaogopa.” Na hayo, kisha nikaanza kumwambia kwamba alikuwa ni nani, na yote kuhusu hilo. Ndipo huyo mvulana nusura aangushe bakuli ya siagi katika sahani yangu.

Kwa hiyo akasema, “Hiyo ni kweli kabisa!”

¹⁵ Mimi, kisha nikamwambia; sio mimi, bali Roho Mtakatifu akamwambia shida ya mke wake nyumbani, na juu ya maombi waliyokuwa wamefanya pamoja asubuhi hiyo kabla hajaondoka, na kusudi lake lilikuwa ni kuniona siku hiyo. Loo, jamani, nusura azimie!

Naye akasema, “Kamwe sielewi jinsi hilo linavyofanyika.”

Nikasema, “Wala na mimi.”

¹⁶ Jambo pekee nijualo ni, Ndugu Shakarian ama... Samahani. Ndugu duPlessis alikuwa tu huko nje kwenye gari nilipoendesha kule, nami pamoja na Ndugu Mercier tulikuwa tukizungumza juu ya roho nzuri kwenye kanisa hili. Tunapenda hilo, ushirika mzuri kweli. Hilo ni zuri sana, ndugu, endelea. Hilo ni zuri sana, ndugu yetu, mchungaji. Na hilo ni zuri. Nasi tulikuwa tukizungumza, nami... Yeye akasema, “Ndugu Branham, nadhani una ninii ngumu sana...”

¹⁷ Nikasema, “La. Jambo linalonishangaza ni neema ya Mungu.” Nikasema, “Nimemaliza rehema Yake, mara nyingi. Lakini kamwe siwezi kuimaliza neema Yake, nami ninafurahia hilo sana.”

¹⁸ Na kwa hiyo wakati tulipokuwa tukizungumza mezani asubuhi hiyo, basi palikuwapo na msichana aliyeshuka akiwa amejifunika shuka begani mwake, akishuka kupitia mahali hapo, akienda kwenye moja ya hizo sebule, kutengeneza vitanda. Nikasema, “Sasa kuna Nuru hiyo inayoning’inia juu ya msichana huyo.” Nikasema, “Mwite tu arudi hapa nyuma.” Ndipo tukamwita arudi. Ndipo Roho Mtakatifu akaanza kumwambia yote kuhusu shida zake.

¹⁹ Naye hakuwa Mkristo; sio mwaminio wa Injili yote, huenda nikasema hivyo. Alikuwa amefanya maungamo, na, wakati alipokuwa mtoto mchanga. Basi mama yake akampeleka kanisani, naye alikuwa na...umri wa miaka kumi na miwili, ama kitu kama hicho. Alikuwa amebatizwa, bali kamwe hakuhudhuria kanisa. Hiyo ndiyo sababu nilisema, “si Mkristo.”

²⁰ Kanisa halikufanyi Mkristo. Kanisa hukusaidia tu kuwa Mkristo, linakusaidia kubaki kile umezaliwa ndani yake,

linakusaidia kushikilia ujuzi wako, wakati unaposhiriki pamoja na ndugu wa Imani moja yenye thamani.

²¹ Ndipo wakati nikiketi hapo, nilikuwa nikiangalia. Naye Ndugu Demos Shakarian akaniita kutoka hapo, na kusema, “Kuna shida gani?” Laiti asingalisema hilo wakati huo!

²² Nikasema, “Kumbukeni, BWANA ASEMA HIVI. Mtu fulani aliye karibu nami, yuko karibu kufa. Pia kutakuwako na kijana mwanamume anayetema damu kutoka kinywani mwake.”

Kisha nikasema, “Yuko wapi Billy?”

²³ Wengi wenu mnamfahamu mwanangu, Billy Paul. Mama yake alikufa alipokuwa ni mtoto mchanga tu. Nami nikambeba kote. Usiku, tusingeweza kumudu kununua makaa ya kutosha kuwasha moto, kwa hiyo tungeninii. . . Ningeweka chupa yake chini ya bega langu, namna *hii*, na kuidumisha ikiwa na joto kwa ajili yake usiku. Wakati angeamka, akimlilia mama yake, ningeitia chupa hiyo kinywani mwake. Naye aliniomba, alipokuwa akifa, “Siku zote dumu pamoja na Billy.” Nasi tumekuwa marafiki halisi. Na kwa hiyo popote niendapo, ninamchukua Billy, naye amedumu pamoja nami.

²⁴ Kwa hiyo, basi, Billy alikuwa akijiandaa kupanda kwenda, wanakoita, “Bustani ya Matumaini” kupiga picha kadhaa. Nikamwita, upesi. Nikasema, “Usiende. Jambo fulani liko karibu kutukia.”

²⁵ Mara nyingi, maono husema mambo tusiyoyajua. Manabii wa Biblia hawakujua waliyokuwa wakiandika, waliyaandika tu. Nao walikuwa ni watu waliothibitishwa, waliovuviwa.

²⁶ Ndipo Ndugu Shakarian akasema, “Ndugu Branham, unasema ni jambo gani litakalotukia?”

²⁷ Nikasema, “Sijui. Mtu fulani, hawakuwa na meno yoyote, nami niliwaona wakihema mara mbili, kisha wakafa. Naye huyo mtu mwingine, walisema. . . alitema damu kutoka kinywani mwao, alionekana kama ni kijana mwanamume; kisha kasema, ‘Hawezi kufa, hayuko tayari.’”

²⁸ Kisha tukaangalia. Nami nikajisikia kuongozwa kwenda Jamaica, bali si Puerto Rico.

²⁹ Kwa hiyo, tulipopata wakati, wakati ulipowadia wa kwenda Puerto Rico, mahali pale pale ambapo ile ndege iliangukia huko Jamaica na kuwaua watu hao wote. Walionekana tu kama nguruwe wakining’inia kwenye mkanda wa usalama, viungo tu vya miili yao vimechomeka kabisa. Na wakaisukuma wakaiondosha, nasi. . . Pale, ndege ingali iko pale tulipoingia. Nayo ndege yetu, ikirudi kutupeleka Puerto Rico, iliunguza pistonni zake kabisa, mahali pale pale, walipotua kutuchukua. Billy askasema, “Baba, una hakika tunapaswa hata kubahatisha kwake?”

³⁰ Nikasema, “Tawi la Wafanyabiashara Wakristo lilisema sina budi kuja. Ni kwa ajili ya ushirika wa tawi hilo ninaenda siku hizi chache usiku.”

Akasema, “Unakumbuka lile ono?” Nikasema, “Naam.”

³¹ Lakini siku tatu baadaye, nilipopata... Nilikuwa nimesimama katika, ... bustani (sijapata kuona kitu chochote cha kupendeza hivi) huko Puerto Rico. Ndugu Fred Sothmann (huenda akawa hapa usiku wa leo), rafiki wa Canada, alikuwa akipiga picha. Nayo hii kubwa... mnayo. Ni nzuri hapa Phoenix, ni nzuri huko Los Angeles, ni nzuri Miami, bali isingefananishwa na ya Puerto Rico. Loo, inapendeza, wala sijapata kuona kitu chochote kama hicho maishani mwangu! Hiyo miamba mikubwa, imetokezea huko, jamani, nusu maili huko nje. Na ndege-korongo wakitembea huko katika bustani za tropiki, na kadhalika. Wala sijapata kuona chochote kinachofanana hivyo na Mbinguni. Ndugu Sothmann akageuka, akasema, “Ndugu Branham, hapana shaka Mbinguni kunafanana na hapa.”

Nikasema, “Loo, haingefanana, haiwezi ikafananishwa na Mbinguni.”

Akasema, “Loo, hizo, ile bahari kuu!”

³² Nikasema, “Lakini ni kule kutikisika kwa dunia, ndiko kunakosababisha yale mawimbi.” Nikasema, “Lakini Kule kutakuwa kutulivu, yatakuwa yakitiririka kwa utulivu yawezavyo.” Nami nikasema, “Haitakuwa ni ndege-korongo wakitembea kote bustanini, itakuwa ni Malaika wakitembea kote bustanini tunakofanyia ushirika.”

³³ Na mara nikamwona mama mkwe wangu na baba mkwe wangu wakipita karibu nami. Baba mkwe wangu ametuacha sasa kwa yapata miaka minane, kumi. Na, dakika iyo hiyo mama mkwe wangu alikuwa akipita kwenda kukutana naye. Akafa wakati uo huo.

³⁴ Ndipo saa mbili baadaye, nilipofika Miami, nilipiga simu kujua jinsi kila kitu kilivyokuwa nyumbani. Mama mkwe wangu (kibogoyo) akahema mara mbili, akafa. Mwanaye, asiyekuwa tayari kufa; takriban, kidogo ni mlevi; akapasuka, kutokwa na damu, kutokana na kutokwa na damu tumboni mwake, naye akatema tu damu kutoka kinywani mwake, kutoka kwa kila njia.

³⁵ Ndugu Shakarian alinipigia simu hivi majuzi. Akasema, “Ndugu Branham, kamwe sijapata kuwa na kitu kilichonigusa hivyo, kusikia hilo.” Mnaona, ilimbidi kukumbuka hilo ono wakati huo, kulisimamisha, ili isijulikane ilikuwa ni nani, kusudi liwe na jambo fulani kwake kufahamu. Akasema, “Ninaamini hii huduma ndio kwanza tu inanza kutenda kazi.” Na iwe hivyo.

³⁶ Na, papa hapa Phoenix, jambo fulani na litukie ambalo litamvuvia kila mmoja, Roho Mtakatifu aje miongoni mwetu na kufanya jambo fulani litakalotufanya tu tukaze silaha na kujiweka tayari kwa ajili ya Kuja Kwake. Bwana abariki.

³⁷ Sasa, kusudi nisiwaweke kwa muda mrefu, maana mmesimama. Lakini ninyi ni kusanyiko zuri sana, ni—ninaonekana kana kwamba ningeweza kuzungumza usiku kucha. Bali sitafanya hivyo, sidhani, lakini nadhani jana usiku mliwazia nilikuwa nikijaribu kufanya hivyo.

³⁸ Nitawapa tu fununu ndogo. Nilizungumza juu ya somo fulani hivi majuzi asubuhi, kwenye maskani yangu, nikaanza kwenye saa tatu na nusu, ndipo nikamalizia yapata saa sita u nusu; niliwaambia hapo kabla, ingawaje; juu ya: *Kusikia, Kutambua, Na Kutenda*. Labda Jumapili moja alasiri, ama kitu kama hicho, huenda tukaliingilia somo lilo hilo. Kwa yapata mwaka mmoja, Roho Mtakatifu amekuwa akishughulika nami kuhusu kulizungumzia, ndipo hatimaye nikalizungumzia kanisani. Nasahau ni kanda ngapi vijana walikuwa nazo juu yake kabla hatujaondoka, kuzichukua.

³⁹ Hebu tufungue sasa kwenye Biblia zetu, upesi, kwenye mlango wa 7 wa Mathayo Mtakatifu, na (sisi) hebu tuanzie kwenye kifungu cha 24.

Basi, kila asikiaye haya maneno yangu, na kuyafanya, Nitamfananisha na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba:

Mvua zikanyesha, mafuriko yakaja, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile; isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba.

Na kila asikiaye hayo maneno yangu, asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga:

Mvua zikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile; na...ikaanguka: nalo anguko lake lilikuwa kubwa.

⁴⁰ Bwana na aongeze baraka Zake sasa kwenye kusomwa kwa Maneno Yake. Nataka kunena kwa dakika chache juu ya somo la *Dhoruba Ijayo*. Nami ninamtumainia Mungu ya kwamba tutaweza kujisalimisha kwa Roho Mtakatifu. Kwa kuwa, mtu yeyote anajua ya kwamba mimi si mhubiri. Hiyo ni kusema, wapo wahubiri nyuma yangu hapa. Kamwe sikupata elimu kuwa mhudumu. Lakini kwa maskini njia zangu za kale, za polepole, bali mimi. . . Bwana alinipa kitu kingine cha kufanya. Ila napenda kuchukua wakati nipate kuelezea yale ninayojua kumhusu Bwana na—na kuhusu wema Wake, na kujaribu kuwaambia wengine kulihusu. Na sasa tunazungumza usiku wa leo juu ya *Dhoruba Inayokuja*. Na kama nikishindwa, katika

maneno, kuelezea yale ninayohisi moyoni mwangu, naomba Roho Mtakatifu atalifunua.

⁴¹ Yesu alikuwa akizungumza hapa juu ya dhoruba ijayo ambayo haina budi kumpiga kila mwanamume na kila mwanamke aliyezaliwa katika ulimwengu huu. Hakuna njia kabisa ya kuiepukia. Dhoruba hiyo itakupiga siku moja ama nyingine. Na inategemea una msingi wa aina gani, kama nyumba yako itaistahimili, ama haitaistahimili.

⁴² Kumekuwako na maisha mengi yaliyookolewa kwa sababu ya maandalizi kwa ajili ya dhoruba. Pia kumekuwako na maisha mengi yaliyopotezwa kwa sababu ya kukosa kuzingatia maonyo juu ya dhoruba zijazo.

⁴³ Sio muda mrefu uliopita, niliambiwa kuhusu hadithi iliyotukia, ninaamini niliisoma katika gazeti huko chini Florida.

⁴⁴ Wana dhoruba nyingi kuu zinazopitia Florida, vimbunga vinavyotokea baharini, na kuyaleta maji (kwa majengo kadhaa ya mji) mjini, na kufagilia mbali kila kitu. Nami nasikia ya kwamba manabii wao wa hali ya hewa sikuzote wako macho kwa ajili ya dhoruba kama hizo. Na njia fulani, kupitia e—elementi hizo, kwamba wanaweza kujua mabadiliko ya hali ya hewa na angahewa, kwamba, hali hii ya hewa inakusanyika namna gani, ambayo itasababisha moja ya hizo dhoruba; kwa sababu wameifanyia mafunzo ya maisha, na kwa vyombo fulani na kadhalika ambavyo sayansi imewaletea. Na kwa kupiga simu awali, na kwa kusikia dhoruba inapitia njia gani, kwamba ina kiasi gani cha upepo; dhoruba zingine zinapitia njia gani, hizo pepo, kama zinaweza kupambana, kuisukumia mbali hiyo dhoruba.

⁴⁵ Ningeweza kusimama hapa na kuhubiri saa moja juu ya hilo, ya kwamba inahitaji dhoruba kubwa zaidi inayokuja, inahitaji upepo mkubwa zaidi kuipindua dhoruba hiyo. Na ndivyo ilivyo siku hizi! Nasi sote tunajua tuna dhoruba ijayo. Nao Upepo pekee niujuao, unaoweza kupindua dhoruba hiyo, utakuwa ni ule Upepo uendao kasi ulioshuka kwenye Siku ya Pentekoste. Nasikia kunao watu hata mjini sasa, wanaozungumza dhidi ya ukomunisti, nao inawapasa kuuzungumzia. Lakini, kuna tu dhidi yake hakutoshi, inatubidi kujua jinsi ya kukigeuza kitu hicho. Halafu kuna kitu kimoja tu kinachoweza kuigeuza dhoruba hiyo, na, hicho ni, Dhoruba yenye nguvu zaidi inayoweza kuishambulia na kubadilisha mkondo wake.

⁴⁶ Nao manabii hawa wa hali ya hewa huko Florida ni hodari sana kwa utabiri wao. Wamewekwa kwa kusudi hilo, kuwaonya watu.

⁴⁷ Nilikuwa nikisoma, ninasahau sasa, ninaamini ilikuwa katika gazeti, juu ya dhoruba miaka michache iliyopita, iliyokuwa njiani kupitia Florida, Florida ya kati, na maeneo yote huko Okeechobee yali—yalionywa. Ndio kwanza nitoke

huko majuma machache yaliyopita. Basi kulikuwako na jirani mmoja aliyendelea kuisikiliza redio wakati wote, kwa sababu ya dhoruba hizi, naye alikuwa ni Mkristo maarufu sana. Basi akasikia ya kwamba kimbunga kikubwa kilikuwa kikielekea huko, kikiinyongayonga miti, na kila mtu alionywa kuingia kwenye usalama.

⁴⁸ Ndipo akawazia juu ya jirani yake aliyekuwa amefuga kuku, na mijengo kadhaa dhaifu iliyokuwa na kuku ndani yake, nyumba zao za kuangulia, na kadhalika, na vizimba vyao. Ambako, yote waliyokuwa nayo maishani yalifungamanishwa na kuku hawa, riziki yao. Basi akakimbia upesi, kiwazimu, hata langoni, ndipo akalisisimamisha gari lake akaruka nje, na kumwambia jamaa huyu, “Wachukue kuku wote ukawaweke kwenye hifadhi yako ya dhoruba, nawe ukimbie kwangu, kwa sababu kimbunga ama dhoruba inakuja ambayo itaangusha kila kitu chini.”

⁴⁹ Ndipo huyo mtu akasimama na kumwangelia usoni, na kumcheka, na kusema, “Upuuzi! Nimewasikia wakitabiri mambo kama hayo awali, nayo hayakutukia kamwe.”

⁵⁰ Naye huyo jirani Mkristo alikuwa amesisimkwa sana, akasema, “Lakini vipi kama likitendeka?”

⁵¹ Tunasikia matamshi kama hayo, njiani, “Nimesikia *hili* litatukia, na *lile* litatukia.” Lakini litatukia moja ya siku hizi! Na inatupasa kusikiliza kila onyo.

⁵² Lakini mtu huyu akasema, “Sina wakati kwa ajili ya ujinga kama huo. Nafuga kuku, wala sina wakati wa kitu kama *hicho*.”

⁵³ Naye akapaza sauti! Huyo jirani akasema, “Katika Jina la Mungu,” akasema, “achana na kuku hao basi, John, uje upesi, wewe na familia yako. Endapo hutaki kuamini hilo, acha familia yako ije.”

⁵⁴ Akasema, “Sitawaruhusu watoto wangu kulisimkwa na maonyo machache ya redio. Mimi na watoto wangu tumeamua tutaishi jinsi niishivyo mimi. Naye mke wangu atanisikiliza mimi kwa kuwa mimi ndiye mlishaji familia hii, naye hana budi kunisikiliza. Mimi ndiye bosi hapa, wala sitawaruhusu watoto wangu wasisimkwe ama kuvurugika sana na upuuzi fulani.”

⁵⁵ Ndipo huyo jirani akageuka, Naye akaenda nyumbani mwake, kwenye kimbilio lake.

⁵⁶ Ndipo, kwa ghafla, mawingu yalikuwa juu yake kabla hawajajua! Hivyo ndivyo hukumu inavyopiga. Inakuja kwa ghafla sana, unashangaa jinsi inavyoweza kufika huko upesi hivyo. Jinsi ambavyo nimewaona watu katili, ambao wakati mmoja walimlaani Mungu, wakianguka na kupiga mayowe, na kusema, “Ungewezaje kunifanyia hivi?” Wote, msingi wote ulifagiliwa mbali kutoka chini yake katika dakika moja. Ina faida kusikia onyo.

⁵⁷ Loo, huenda mkamcheka mjumbe, huenda mkaweza hata kumwua. Lakini, hamwezi kuua Ujumbe, utaendelea vile vile tu. Ujumbe wa Mungu ni wa Milele. Maneno Yake kamwe hayatashindwa.

⁵⁸ Paulo alifanikiwa katika kumfanya Stefano apigwe mawe. Lakini kote katika maisha yake, mpaka alipojisalimisha kwa Kristo, kamwe hakuweza kuuondokea Ujumbe huo, “Naona mbingu zimefunguka, na Yesu amesimama mkono wa kuume wa Mungu.” Kitu fulani kilimshika. Haikuwa ni yule mjumbe, ilikuwa ni Ujumbe aliokuwa nao.

⁵⁹ Wakati dhoruba ikivuma kote nchini, iliishika hiyo nyumba ya kuku na yule mkulima, wala hawakuupata mwili wake.

⁶⁰ Naye mkewe, akipambana kiwazimu. Nao waliishi karibu na Ziwa kuu la Okeechobee, ndipo maji yakaanza kupanda wakati kimbunga kilipoyainua hayo maji kote kutoka chini ya ziwa. Hilo ndilo linaloyafanya hatari sana; yana kina kifupi, mashua huyumbayumba, na hivyo ndivyo mawimbi hupanda juu na kuzipindua mashua chini yao. Dhoruba huja na kuyazungusha-zungusha maji kasi na kuzibeba maili kadhaa. Nayo maji yanaenda kasi, mpaka, mama alijua hapakuwapo na matumaini ila kuwapandisha watoto juu ya hilo jengo. Basi akawachukua watoto wake, na kuwaweka juu ya hilo jengo, wakishikilia juu ya dohani ya hiyo nyumba.

⁶¹ Ndipo wanyama mwitu, Nyoka wa Majini mwenye sumu, ninaamini, nyoka aliye hatari kuliko Nyoka Mtatarika mwenye madoa ya almasi. Walikuwa wakitambaa wapate usalama, nao wakaja paani pamoja naye. Na kwa kumsikiliza mumewe, pasipo kusikia onyo, ilimbidi... alifanya vishindo na kupiga, bali ilimbidi kusimama na kuwatazama hao nyoka wakali sana wakiwaua watoto wake hata wakafia kwenye paa. Naye mama mwenyewe aliumwa sana hata hatimaye akafa, hivyo ndivyo tu tulivyoipata hadithi hiyo. Baada ya hiyo dhoruba kutulia, nacho kikosi cha kutafuta kikiitafuta miili, na kadhalika, walimkuta amelala juu ya paa, huku watoto wake wamelala kando yake.

⁶² Loo, ina faida kutii onyo! Jambo la kwanza kufanya, kabla hapajaweza kuwa na onyo, hapana budi pawe na maandalizi yanayofanywa kwa ajili ya usalama, la sivyo hakuna haja ya kutuma onyo. Nalo onyo ni sauti tu ya mtu kukufanya ujiandae kwa ajili ya hatari. Hapana budi pawe na maandalizi yaliyofanywa kwanza. Ndipo basi kama maandalizi yamefanywa, basi onyo linaweza kutolewa kukufanya ufanye uamuzi wako mwenyewe, kama unataka kulisikiliza, au la. Kama hutaki kulisikiliza, vema, hiyo ni juu yako. Kama ukilisikiliza, kuna usalama.

⁶³ Mungu ana utaratibu uo huo. Tunafanya kazi kwa utaratibu wa Mungu, kwa njia hiyo. Mungu, katika siku za mwanzoni, wakati ulimwengu uliotangulia ile gharika, wakati watu

walipokuwa waovu na wenye dhambi sana, hata Mungu asingeweza kuangalia jambo hilo na kuwa mwenye haki.

⁶⁴ Mungu ni mwenye haki, Naye ana sheria. Wakati sheria hizo zinapovunjwa. . . Sheria yoyote inayovunjwa, isiyo na adhabu, si sheria. Huwezi kuzivunja sheria za Mungu bila kulazimika kuzilipia mahali fulani. Huna budi kufanya hivyo. Biblia ilisema, “Uwe na uhakika dhambi zako zitakupata.”

⁶⁵ Nayo dhambi ni nini? Ningetaka kusimama hapa kwa dakika moja tu. Watu wengi wanafikiri kuvuta sigara ni dhambi. Sivyo. Watu wengi wanafikiri ya kwamba kusema uongo ni dhambi. Sivyo. Kufanya uzinzi, hiyo si dhambi. Hiyo ni matokeo ya kutokuamini. Wewe, sababu ya wewe kufanya mambo hayo ni kwa sababu wewe ni asiyeamini.

⁶⁶ Kuna mambo mawili tu, hayo ni, ama wewe ni mwaminio au si mwaminio. Endapo wewe ni mwaminio, hufanyi mambo hayo. Kama wewe huyafanya, sijui una maungamo ya namna gani; lakini, kama ukifanya hivyo, “kumpenda Mungu hakumo ndani yako.” Biblia ilisema hivyo! Tuna maungamo mengi kupita kiasi pasipo umilikaji wake; misemo mingi kupita kiasi, huku hatuiishi.

⁶⁷ Nadhani, hata, tuna mazoezi mengi sana ya mahubiri, huku hatuyaishi mahubiri ya kutosha. Ingekuwa ni bora zaidi kama tuliyaishi mahubiri yetu, kila mmoja wetu angekuwa mhudumu. Ni afadhali uniishie mahubiri kuliko kunihubiria moja. Biblia ilisema hivyo, “Ninyi ni nyaraka za Mungu zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote.” Kwa hiyo, ni bora zaidi kuyaishi mahubiri.

⁶⁸ Dhambi ni kwa sababu huamini. Hivi Yesu hakusema, katika siku za mwili Wake duniani, hivi Yeye hakuwaita. . . Watu ambao wasingesema uongo, ambao wasingeiba, ambao wasingefanya uzinzi, watu wenye haki, wahubiri, makuhani, Yeye alisema, “Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi,” kwa sababu hawakumwamini Mwana wa Mungu. “Yeye asiyeamini amehukumiwa tayari.”

⁶⁹ Siku moja, nililifanya, nikifanya miito ya madhabahuni. Ninapenda Yohana 5:24. “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele; wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Yeye aaminiye!

Kasema, “Hilo ni rahisi sana.”

⁷⁰ La, hilo lina kilindi sana, kwa kuwa, “Unapoamini!” “Hakuna mtu anayeweza kumwita Yesu ‘Kristo,’ ila kwa Roho Mtakatifu.” Unapokuwa na Roho Mtakatifu, basi umeamini hata kwa Uzima wa Milele, nawe unao Uzima wa Milele. “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele; wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Maandalizi, kujiweka tayari!

⁷¹ Naye Mungu aliona uovu wa ulimwengu, na kukiona hicho kizazi kiovu na cha zinaa, wala utakatifu Wake usingeweza kukivumilia zaidi.

Loo, kwa ulimwengu huu wenye dhambi!

⁷² Nilisimama hivi majuzi, nikiwa njiani kwenda kwenye duka la vyakula, pamoja na mke wangu. Nasi tulikuwa tukizungumza kuhusu msichana fulani wa mji wetu. Hali baridi sana ya hewa; naye amevaa koti dogo nene, na amevalia kizinifu, pamoja na maskini zile kaptura, ambazo wanavaa msimu wa kiangazi; kukiweko na malundo ya barafu ardhini. Ndipo mke wangu akasema, “Unajua mwanamke huyo hawezi kuwa na starehe.”

Nami nikasema, “La. Ni kwamba tu hana akili timamu.”

Naye akasema, “Vema, unajua yeye huenda shule ya upili.”

⁷³ Ndipo nikasema, “Huenda akaenda kwenye shule ya upili, bali hilo bado halifanyi kila kitu sawa.” Nikasema, “Hawezi kuwa ana akili timamu.”

⁷⁴ Tunapoingia Ujerumani. Nilikuwa Ujerumani wakati fulani uliopita, kwenye mkutano mkubwa ambako Bwana alikuwa akitupa yapata... yapata nafsi elfu kumi, kila usiku. Nami nilishangaa sana usiku mmoja nilipotoka mkutanoni, na—na chini barabarani nikienda mahali nilipokuwa nimealikwa kwa ajili ya chakula kidogo cha mchana. Na ilikuwa ni kwenye kumalizia kwa huo mkutano, nao Wakristo wote wameketi pande zote, wakinywa pombe. Vema, Marekani, Canada, na Uingereza, ndiyo mataifa pekee nijuayo ambayo huwakataza Wakristo kunywa pombe. Hawalewi; bali sisi Wamarekani. Ndipo wakati... Mimi sikuinywa. Kwa hiyo, baada ya kitambo kidogo, swali lilizuka mezani, “Kulikuwa na nini,” kwamba sikuwa nikinywa pombe yangu, “ni kwamba haikuwa nzuri?”

⁷⁵ Ndipo Dakitari Guggenbuhl aliyekuwa ameketi karibu nami, ambaye alikuwa mkalimani wangu. Nikasema, “Kwa nini wote wananung’unika, kwangu?”

Naye akasema, “Wanashangaa ni kwa nini wewe hunywi pombe.”

⁷⁶ Sasa, ninajua imeandikwa: ukiwa Rumi, kuwa Mrumi. Lakini nikasema, “Waambie hivi: ‘Siwahukumu. Bali nilizaliwa Mnadhiri, sipaswi kunywa pombe.’” Sikutaka kuwaudhi. Nao wakaelewa, wakaendelea tu kunywa pombe.

⁷⁷ Halafu basi huko Italia tulipata karibu jambo lile lile. Na sehemu nyingi mbalimbali za ulimwengu, unapoingia katika mataifa, unapata roho ya hilo taifa.

⁷⁸ Ninakumbuka Roho Mtakatifu akinionya nisiende kwenye YMCA huko Finland. Sikujua ilikuwa ni juu ya nini. Nikaja kugundua, walikuwa na wanawake waogeshaji kule. Basi sikuenda, wala nisingeingia pamoja na Dakitari Manninen na hao wengine, kuogelea. Ndipo nikagundua, wanawake hao

wasugua waliwasugua wanaume. Nami nikasema, “Hilo si jambo zuri!”

⁷⁹ “Vema,” akasema, “Ndugu Branham, hiyo ni sawa tu kadiri ilivyo kwa wauguzi wenu huko Marekani.” Kasema, “Wamefunzwa kufanya hivyo.”

⁸⁰ Nikasema, “Sijali wamefunzwa jinsi gani, kamwe haikukusudiwa hivyo! Mungu aliwafunika, na kuwafanya tofauti!” Kweli! Bali hawajali Hilo.

⁸¹ Walikuwa ni Wafini, watu wazuri sana, bali ni roho ya hilo taifa. Popote uendapo, unapata roho ya hilo taifa. Ndipo unakuja Marekani, umeipata kweli basi, hiyo ndiyo mbaya zaidi kuliko zote.

⁸² Naye mke wangu akaniambia, “Mbona, hao watu huenda kanisani, nami mara nyingi nimeshangaa ni kwa nini haikuhukumu dhamira yao.”

Nikasema, “Mpenzi mke wangu, hebu nikwambie. Hao ni Wamarekani.” Akasema, “Vema, mbona, na sisi je?”

⁸³ Nikasema, “La.” Nikasema, “Tunaishi tu hapa. Bali tumezaliwa kutoka Juu, Roho Mtakatifu wa Mungu alishuka juu yetu.”

⁸⁴ Kwa hiyo, sisi ni wasafiri na wageni hapa, hapa si mahali petu pa kudumu. Bali tunautafuta Mji ujao, Ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni ni Mungu. Kwa hiyo unapozaliwa kutoka Juu, unaye Roho Mtakatifu akishuka kutoka kwa Mungu, anayeibadilisha asili yako. Haidhuru, dada yako, mama yako, rafiki ya—yako aliye mzuri sana angeweza kuvalia namna hiyo; bali Mkristo aliyezaliwa na Roho wa Mungu, amezaliwa kutoka Juu, nayo Royo yao ni ya Ufalme mwingine. Loo, nina furaha sana kwa hilo! Ule urahisi wa Roho Mtakatifu; kumfuata, kumwangalia, jinsi anavyotenda, anavyokufanya utende.

⁸⁵ Hivyo ndivyo ilivyokuwa katika siku za Nuhu, naye Mungu akachoshwa sana nayo! Lakini kabla Yeye hajaituma dhoruba kuuangamiza ulimwengu mzima, Mungu alifanya maandalizi kwa ajili ya wale waliotaka kuikwepa. Nami ninaweza kumwona Nuhu akisimama mlangoni pa safina, akihubiri haki. Loo, hapakuwapo na wengi wangalimsikiliza.

⁸⁶ Walikuwa kitu kama leo hii. Wanataka burudani, sio Injili. Ole wao wainjilisti hawa wa Hollywood wanaogopa kuita dhambi “dhambi!”

⁸⁷ Tunahitaji baadhi ya wahubiri wa mtindo wa kale, wa nyuma ya misitu walio na Roho Mtakatifu, wasioogopa kuihubiri Injili kwa mikono yao mitupu, isiyofunikwa na namna fulani ya glavu za mpira; lakini kuhubiri Kuja kwa Bwana Yesu, hukumu kwa ajili ya waovu, na Mbinguni kwa ajili ya wenye haki, na kule kukaribia! Msimu gani? Sijui, wala hakuna mwingine ajuaye.

Lakini nitakionya kizazi changu. Kama ikija sasa, ninawataka waonywe.

⁸⁸ Ninaweza kumwona Nuhu katika mlango wa safina yenyewe. Loo! Ningetaka tu kuamini jambo moja, haikuwa hivyo; bali Nuhu akisimama kwenye mlango huo, njia pekee ya usalama.

⁸⁹ Ninaweza kumwona Musa, baadaye, amesimama mlangoni, pamoja na damu kwenye kizingiti, akihubiri hukumu, pamoja na damu kwenye kizingiti.

⁹⁰ Leo hii, Yesu ndiye Mlango wa zizi la kondoo, wahudumu wa Injili wakisimama kwenye huo Mlango, wakilisihi kusanyiko lije kwenye usalama.

⁹¹ Na hapana shaka ila kuna wengi waliomcheka Nuhu, wakamdhihaki. Biblia ilisema, “Walikuwa wenye dhahaka.” Ninaweza tu kuwasikia wakisema kitu kama hiki, “Nuhu, kama huna burudani nzuri kuliko hiyo, tutakaa tu nyumbani.”

⁹² Ulimwengu siku hizi, Marekani, haitaki Injili. Wanataka burudani. Hawana budi kuwa na kitu cha kuwatumbuiza; muziki mwingi wa kuvutia, ama kitu kama hicho, ama namna fulani ya karamu, namna fulani ya nyama choma. Ambapo, mambo hayo yote ni sawa, nje ya kanisa. Bali kanisani ndiko hukumu inapaswa kuhubiriwa katika Nguvu za kufufuka kwa Bwana Yesu, na onyo. Hukumu huanza kwenye nyumba ya Mungu! Sio karamu; hukumu!

⁹³ Lutu alionywa. Ndipo wakati wale Malaika, ingawa hakujua walikuwa ni Malaika, waliposhuka, ujumbe wao ulikuwa kwa Sodoma, “Ondokeni mahali hapa pa dhambi! Mungu ameweka njia ya kuepukia kwa ajili yenu. Ondokeni mahali hapa pa dhambi!”

⁹⁴ Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.” Agalieni waliishi maisha ya namna gani. Naye Yesu aliilinganisha siku hiyo na hii. Yenye dhambi!

⁹⁵ Angalia wakati Lutu alipotoka kwenda kuwaambia watu wake. Walimcheka, wakamdhihaki. “Nazo dhambi za huo mji, ziliitesa roho yake yenye haki.” Ujumbe wa Malaika haukuwatikisa, haukuwa na matokeo kwao. Bali waliombwa watoke, kwa sababu hukumu ilikuwa juu ya huo mji, naye Mungu alikuwa alete dhoruba ya moto juu ya huo mji. Nao wakakataa kutembea. Wakakataa kutoka. Waliridhika na dhambi zao.

⁹⁶ Watu siku hizi wanaonekana kuridhika sana katika dhambi, kwa sababu tuna gari jipya, kwa sababu tunaweza kula milo mitatu kwa siku, tulale kwenye kitanda safi. Hilo ni zuri sana. Lakini, hilo lingekuwa ni zuri, lakini tunamsahau Mungu wakati mafanikio yanapokuja jinsi hiyo. Nafikiri tumekuwa hivyo. Sisi wahubiri na sisi Wakristo tumevutiwa sana kwenye—kwenye

miradi ya ujenzi wa makanisa yetu na kupata kanisa bora zaidi, ama kitu kama hicho, ama kanisa kubwa zaidi, viti bora zaidi. Ama, mnajua jinsi na kile ninachomaanisha. Nasi tumeacha lile jambo muhimu: hukumu, haki, Nguvu za Roho Mtakatifu, ufufuo, hukumu ya Milele.

⁹⁷ Malaika kamwe hakushindwa kuuhubiri huo ujumbe. Ingawa walijaribu kuwazuia, lakini ujumbe Wao uliendelea vivyo hivyo.

⁹⁸ Sasa, uliona, ni kama tu mtu anayesema, “Nitakataa kuamini jua linawaka. Sitakuwa na uhusiano wowote na jua.” Anayafunga macho yake, kisha anashuka kwenye chumba chake cha chini ya nyumba yake, kisha kasema, “Nakataa katakata kujua jua linawaka.”

⁹⁹ “Mbona,” mnasema, “Ndugu Branham, mtu huyo, angekuwa na kasoro fulani ya akilini.”

¹⁰⁰ Vema, mtu atakayemkataa Yesu Kristo, ana misingi iyo hiyo. Roho Mtakatifu ni halisi zaidi kuliko mwanga wa jua. Jua litashindwa, bali Roho Mtakatifu hawezi kushindwa. Hamuliki tu kwa ajili ya hisi ya kuona, bali humulikia kwa ajili ya nafsi, Nuru ya utukufu unaotungoza kwa Mungu, unaokataa... ama kutuonyesha, hasa, Kalvari, na mateso ya Bwana Yesu; hukumu ijayo, na wokovu kwa wale wanaotaka kuja. Afadhali niwe kipofu kabisa, kimwili, na niwe na macho yangu ya kiroho; kuliko kuwa kipofu kabisa, kiroho, na kuwa na macho yangu ya kawaida. Ninataka kuwa na macho ya kiroho.

¹⁰¹ Angalieni, huyo mtu angekuwa na shida gani? Hao, marafiki zake, wangukuwa na kusema, “Jim,” John, ama lolote lililo jina lake, “umekosea. Toka kwenye chumba hicho cha chini chenye giza-giza, kichafu.”

¹⁰² Naye angesimama na kusema, “Nitawaambia, nimeridhika mahali nilipo!” Hataki mwa—mwanga wa jua uliokaribishwa. Hataki miale yake yenye kuponya. Hataki uzuri wake, joto la—lake kwa ajili ya maisha yake. Mtu huyo angekuwa na kasoro fulani.

¹⁰³ Vivyo hivyo na mwanamume ama mwanamke anayetaka kukaa kwenye ulimwengu wenye giza-giza, amefungiwa katika uchafu wa dhambi ya kutokuamini, na kusema, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu. Hakuna Roho Mtakatifu.” Ni kwa sababu unakataa kutoka kwenye uchafu na matundu ya ibilisi, na ya kuzimu, na ya dhambi, na ya kiburi.

¹⁰⁴ Tembea katika Nuru ya Injili, ambayo itakuletea joto! Loo, ni faraja jinsi gani! Kuona hukumu zijazo, na kuhisi hisia hiyo ya faraja ya Roho Mtakatifu! Mnawasikia wakizungumza juu ya mabomu ya atomiki? Basi wazieni tu kile kilichotukia, amani ipitayo ufahamu! Mbona, bomu halitakuwa limetoka kwenye bunduki kabla hatujawa Uweponi mwa Yesu, tukiwa na Uzima wa Milele; sisi wazee, turudi kuwa vijana tena; watoto wachanga,

waufikie umri fulani; pasipo na mauti tena wala huzuni. Loo! ni jambo la ajabu jinsi gani! Unamaanisha mtu anaweza kukataa kutoka na kutembea katika Hiyo? Huyu mtu ana kasoro.

¹⁰⁵ Hatimaye, kama hatapata mwanga wa jua, anapata mpauko. Anapauka kabisa, anashikwa na ugonjwa.

¹⁰⁶ Hiyo ndiyo shida ya ulimwengu siku hizi. Hiyo ndiyo shida ya karibu makanisa yetu yote siku hizi. Tunashikwa na anemia. Tunahitaji nyongeza ya damu. Tumepauka, kwa sababu tunaugua, afya yetu ya kiroho inazorota. Hatuna juhudi tena, kutafuta nafsi, ku—kuwaonya watu, kuwaleta majirani zetu, kuwaleta marafiki zetu, mwuza maziwa, mvulana mwuza magazeti. Hata iweje, mlete mtu kwa Bwana Yesu! Tumepauka; tunashindwa kutembea Nuruni, ambako ni majaliwa yetu; kushindwa kuamini katika afya ya Mungu, kwa uponyaji wa Kiungu.

¹⁰⁷ Ninaambiwa katika Biblia ya kwamba utakuja wakati, kwa wale wasio kwenye Nuru hii ya ajabu ya Mwana, ya kwamba ndege wa angani wataila miili yao; kwamba magonjwa yako njiani, ambayo madaktari kamwe hawataweza kukomesha. Ni mapigo ya Mungu.

¹⁰⁸ Madaktari wa Misri, ambao walikuwa ni werevu sana kuliko wetu siku hizi, wasingeweza kuyakomesha mapigo ya Mungu, wala wachawi wao wala waigaji wao. Ilihitaji Gosheni, na Nguvu za Mungu, kuwashikilia watu Wake; chini ya damu ya mwana-kondoo!

¹⁰⁹ Roho Mtakatifu ndiye Mlango huo leo hii. Roho Mtakatifu ndiye usalama huo leo hii.

¹¹⁰ Nilikuwa kwenye mkutano si muda mrefu uliopita. Ninamtaazama ndu—ndugu mweusi anayeketi hapa, nadhani, yeye na mke wake. Nami nimekuwa nikimtaazama tangu nimekuwa nikihubiri, akitikisa kichwa chake, na kufurahia kwenye mkutano. Ndipo likanileta tu kwenye wa—wazo fulani.

¹¹¹ Kulikuwako na mvulana aliyekuja mkutanoni, wakati mmoja. Na mara ibada ilipokwisha, akanikimbilia, na kusema, “Kasisi!” Alikuwa Mkusini. Basi akasema, “Kasisi, ninataka kumpata Bwana Yesu, usiku wa leo.” Nilikuwa nikifanya ibada ya uponyaji.

¹¹² Nami nikasema, “Bila shaka, ndugu yangu, mimi nina furaha hata na zaidi kukuongoza Kwake.”

¹¹³ Akasema, akiisha kumpa Bwana moyo wake, akasema “Sijui, nadhani unashangaa ni kwa nini nilikimbia, hapa nje namna hii.” Kasema, “Nilisikia ulikuwa mjini, nami nikaja tu kuona nini, kukuona wewe.” Akasema, “Nitakwambia hadithi yangu.” Akasema, “Nimekuwa, takriban, mzururaji.” Kasema, “Mama yangu mzee alikuwa Mkristo halisi. Dada zangu walikuwa Wakristo. Nina ndugu mmoja Mkristo.” Kasema,

“Nilikuwa, kitoto kichanga cha familia, na mtoto aliyeharibika, kwanza kabisa, maana walinidekeza, walikuwa wazuri sana kwangu.” Lakini akasema, “Nisingemsikiliza mama yangu wala jamaa zangu watauwa. Nilitaka kuwa mzururaji. Nilitaka kuishi ‘maisha ya mwanamume.’” Akasema, “Nilidhani kwamba kuwa Mkristo ilikuwa zaidi sana ni kwa wanawake, ama wanyonge.” Akasema, “Basi nikawa mpishi, nami nilikuwa mzuri sana kwa kazi yangu.”

¹¹⁴ Kisha akasema, “Jambo moja, ama lingine, nilitaka kwenda Kaskazini. Basi siku moja nikapepesuka nikaingia kwenye kambi ya mbao, walipokuwa wakikata miti ya mbao. Nami nilikuwa nimefilisika. Basi nikamwambia msimamizi, ‘Unaweza kumtumia mpishi?’” Akataja mapendekezo yake, aliyokuwa nayo mfukoni mwake, kutoka mahali mbalimhali pakuu ambako alikuwa mpishi.

¹¹⁵ Kisha akasema, “Vema, tuna mmoja sasa.” Akasema, “Lakini, hata hivyo, mpaka utakapoweza kujitegemea, tunaweza kukupa pesa kidogo za kando. Tunaye mama mkongwe mweusi mle sasa, ambaye ni mpishi mzuri. Lakini ingia, zungumza naye, labda anaweza kukutumia. Na endapo anaweza, tunaweza kukupa pesa kidogo za matumizi mpaka utakapoweza kujitegemea.”

¹¹⁶ Akasema hayo yalikuwa ni mazuri kadiri alivyotaka. Naye akasema aliingia mle, akakutana na huyo mwanamke mkongwe, basi akasema alimsaidia huko kwa siku mbili ama tatu.

¹¹⁷ Basi usiku mmoja, alisema alikuwa amelala kule, naye akasema “Aliendelea kuona vimulimuli vikimulika kando ya ukuta.” Ndipo baada ya kitambo kidogo, akajiuliza, “Kwani, kuna mtu nje?” Kisha kasema, baada ya kitambo kidogo “akasikia ngurumo nzi—nzito, nayo ilikuwa ni ngurumo ya radi.” Kisha kasema, huko nje “akasikia sauti zikizungumza, nazo zikasema, ‘Mwajua, afadhali turudi kwenye farasi, tukawahudumie, kwa sababu huenda tusiwe hapa muda mrefu sana.’” Kasema aliondoa kifuniko kichwani mwake, na kusikilizia ukutani. Ndipo radi ikamulika, naye akamwona bosi wake na masaisi. Ndipo akafahamu, kwa mazungumzo yao, ya kwamba kulikuwa kunakuja dhoruba kupitia milimani.

¹¹⁸ Ambayo tunaita, huko kaskazini, “mkaskazini,” huja upesi, bila onyo. Huna wakati kufanya lolote. Hiyo milima ni mirefu sana, inapasuka tu moja kwa moja, kwa ghafla.

¹¹⁹ Nacho kimulimuli hicho kilikuwa kikimulika. Naye akasema, “Wajua nini, huenda tusiwe hapa baada ya kitambo kidogo.” Kasema, “Hilo linasikika kama tatizo baya sana linakuja.”

¹²⁰ Kisha akasema “Nikaanza kuwazia, ‘Vema, natumaini haitapiga hapa,’ kasema, ‘kwa sababu ninajua siko tayari

kwenda.” Wakati mwingine unangojea muda mrefu kupita kiasi, unajua.

¹²¹ Kwa hiyo basi akasema, “Katika dakika chache tu, upepo ulianza kuvuma, nayo miti ikaanza kutikisika.” Naye akasema alisikiliza. Turubai ilikuwa kati yake na mahali huyo—huyo mwanamke mkongwe alipolala, ndipo akasema, “Alikuwa akiipiga turubai hiyo. Akasema, ‘Mwanangu? Loo, mwanangu?’”

Akasema, “Naam?”

¹²² Akasema, “Waweza kuja huku upande wangu? Nina fanusi inayowaka.” Kisha kasema, “Nilimwendea, kwa maana niliogopa, karibu kufa.” Kisha kasema, “Alikuwa na fanusi imewekwa juu ya sanduku la sabuni lililochakaa. Naye akasema, ‘Ningetaka kukuuliza jambo fulani.’”

Akasema, “Naam, mama.”

Kasema, “Wewe uko tayari kumlaki Bwana?”

Akasema, “Ndipo kweli nikaogopa. Kasema, ‘La, mama, siko tayari.’”

¹²³ “Vema,” akasema, “kipenzi, ninataka uniambie jambo fulani. Afadhali ujitayarishe sasa, maana huenda ikakubidi kukutana Naye, bila ya kujiandaa, katika dakika chache zijazo.” Kasema, yeye alisema, “Waweza kupiga magoti pamoja nami hapa?”

¹²⁴ Kasema, “Tulipiga magoti kando ya sanduku hilo la sabuni lililochakaa.” Akasema, “Kasisi, nitakwambia kweli, niliogopa sana nisingeweza kuomba.” Akasema, “Miti ilikuwa ikiligonga jengo hilo, nayo radi ilikuwa ikimulika, na ngurumo zikitikisa. Niliogopa sana nisingeweza kuomba.” Kasema, “Nikaanza kusema, ‘Bwana, uturehemu,’ ndipo radi ingefanya *twaa*. Ningesema, ‘Nilikuwa wapi? Bwana, uturehemu,’ *twaa* radi ingemulika.”

¹²⁵ Akasema, “Lakini nilijifunza somo.” Akasema, “Maskini mwanamke huyo mtakatifu aliketi mtulivu tu alivyoweza kuwa.” Kasema, “Mwanamke huyo alizungumza Naye kana kwamba alimfahamu tangu alipokuwa mtoto mchanga, kana kwamba alikuwa ni baba yake ama mama yake.” Akasema, “Hakusumbuka hata kidogo.”

¹²⁶ Kasema, “Nilihofu karibu kufa.” Kasema, “Hatimaye, nikatoa maneno haya, nami nikasema, ‘Bwana, kama tu ungeniruhusu kuishi, na nipate mahali ambapo ni patulivu zaidi, nitakuja Kwako.’”

¹²⁷ Akapata nafasi nyingine, lakini huenda wewe usipate. Wakati hukumu za Mungu zitakapoanza kumwagwa, hakuna nafasi tena. Una nafasi yako sasa. Hii ndiyo nafasi yako.

¹²⁸ Dhoruba ilikuwa juu yake! Akasema, “Kasisi, inawezekana kwa mtu kama mimi kufichwa kwenye usalama huo; hata mauti

yatakapoanza kuja juu yangu, nipate kuingia na kuzungumza na Yeye, kama huyo mtauwa mkongwe alivyofanya?”

¹²⁹ Nikasema, “Mwanangu, Damu ya Yesu Kristo, iliyomfanya hivyo, inaweza kukufanya hivyo sasa hivi.”

¹³⁰ Nilikuwa nimesimama karibu na gari langu. Alikuwa ni mvulana aliyevalia nadhifu, mstaarabu, mwenye elimu. Akapiga magoti yake, kwenye kitalu kilichojaa matope; na hapo akapata Mahali hapo pa kujificha, Kimbilio lile katika wakati wa dhoruba, ule Mwamba katika nchi ya uchovu.

¹³¹ Haikubidi kuwa mchovu maadamu uko katika Mwamba. Mwambani ni mahali pamoja pasipo na uchovu. Mwamba ndipo mahali pa kuridhisha. Unaweza tu kuketi na kuangalia nje, salama tu uwezavyo kuwa.

¹³² Ipo saa inayokuja, na sasa ipo, (na kutiwa muhuri karibu kumekwisha), ambapo kila mwanamume na mwanamke kwenye uso wa nchi atakuwa mahali hapo pa Kimbilio, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ama nje Yake. Huna budi kufanya uamuzi wako. Usalama huo ni Yesu Kristo. Kwamba, Yeye ndiye Mahali pekee, Yule pekee aliye na Uzima wa Milele. Hakuna mtu awezaye kuja kwa Baba, ila kupitia Yeye. Yeye ndiye Safina ya usalama wetu. Roho Mtakatifu hushuhudia pamoja nasi sasa, kwamba tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani.

¹³³ Ndipo wakati tunapoangalia kaburini, na kujua ya kwamba kila mmoja wetu anaelekea kule!

¹³⁴ Tunaona magazeti, na dhoruba ijayo! Utakapoenda nyumbani usiku wa leo, nitendee wema, usiende kitandani mpaka utakaposoma Ufunuo, mlango wa 8. Mnaona mapigo yajayo na dhoruba itakayoipiga nchi, na ngurumo na radi vitatikisa mbingu. Ole zitapita juu ya taifa. Wanadamu wataoza katika mwili wao. Magonjwa yatawapiga, madaktari hawajui chochote kuyahusu.

¹³⁵ Lakini kumbukeni, kabla hilo halijatukia, kuna kutiwa muhuri kulikoendelea! Naye malaika wa mauti na mapigo aliagizwa na Mungu, “Usimkaribie yeyote wa hao walio na Muhuri kwenye paji la uso wao!” Nao Muhuri wa Mungu ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Waefeso 4:30 inasema, “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwaye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu.” Haidhuru safina iliyumba kwa nguvu namna gani, haidhuru ni mara ngapi radi ilipiga karibu nayo, “Elfu kumi wataanguka mkono wenu wa kuume, na maelfu mkono wenu wa kushoto, bali hayatawakaribia.” Roho Mtakatifu!

¹³⁶ Nilisoma juu ya, “Mpanda farasi wa kijivu akitoka, ambaye anaitwa ‘Mauti,’ na Kuzimu kulimfuata.”

“Mpanda farasi mweusi mwenye mizani mkononi mwake.”

137 “Kibaba cha ngano kwa nusu rupia, na vibaba viwili vya shayiri kwa nusu rupia, bali usiikaribie Divai Yangu wala Mafuta Yangu!”

138 Ninasikia, kwa Biblia, hukumu za Mungu zijazo, ambapo maradhi, na taabu, na maafa yatayapiga mataifa, na kila taifa litavunjika vipande-vipande. Nilisoma katika Bi-... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

139 Kila kitu kilikuwa kitulivu. Lakini Bwana Yesu akaliiondoa giza kutoka machoni mwake, ndipo akashika ghafla meya wa mji, na kupaza sauti, “Ninaweza kuona! Ninaweza kuona!” Wakati maelfu wakisimama pale, Waislamu, na kadhalika.

140 Nikasema, “Sasa Safina ya usalama ni nini?” Nikasema, “Nilisoma kwenye gazeti lenu, hivi majuzi, ambapo ndege wote wadogo waliozoea kutulia kwenye miamba kuzunguka ua, na kwenye minara mikubwa ya mijengo pembeni.”

141 Mwajua, India ni nchi maskini nao huokota mawe kondeni, na kujenga nyua zao. Nao hao ndege wadogo hujenga viota vyao katika miamba hii, zile nyufa, na kwenye mashimo. Wanaingia humo ndani na kutengeneza viota vyao, watoke kwenye mvua. Na halafu ng’ombe, wote, alasiri, wakati jua linapoelekea Magharibi, mbona, ng’ombe wanasimama kwenye kivuli cha nyua hizi—hizi na minara mikubwa, waingie kwenye kivuli.

142 Lakini, kwa yapata siku mbili, jambo lisilo la kawaida kabisa lilitukia. Maskini ndege wote waliwachukua vifaranga wao, makinda wao wa ndege, wote pamoja, na kuruka kuondoka kwenye hizo kuta, wala hata hawakurudi usiku. Walitoka wakaenda kondeni katikati, kisha wakaketi chini, ng’ombe wasingerudi alasiri. Walikaa mbali na hizo kuta. Ndipo wakakusanyika pamoja, na kusimama karibu sana pamoja hata wakafanyiana uvuli mmoja kwa mwingine.

143 Ndugu, dada, hivyo ndivyo Kanisa linavyopaswa kufanya! Hatuhitaji kivuli cha hizi Babeli ndefu sana siku hizi, za kisasa. Tunahitaji baraka za mmoja kwa mwingine, pamoja, ushuhuda wetu, nao upendo wetu wa Kikristo na udugu uliomininwa mioyoni mwetu na Roho Mtakatifu. Huo unafanya kivuli; wakati ninapoweza kumshika ndugu yangu mkono, nimshike dada yangu mkono, na kujua ya kwamba sisi ni wenyeji wa Ufalme wa Mungu; kwamba tunapendana sisi kwa sisi, na tunasimama pamoja katika Huduma hii moja kuu, Huduma ya Kristo. Kama wewe ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, Umoja, Uwili, Utatu, chochote ulicho, haileti tofauti yoyote, mradi tu Damu ya Yesu Kristo inatusafisha na dhambi zote nasi tuna ushirika sisi kwa sisi. Hilo ndilo tunalotaka, udugu, ushirika!

144 Walisimama makondeni. Walikataa kusimama kwenye kivuli cha kuta. Watu walidhani hilo lilikuwa ni la kigeni. Lilikuwa ni tendo la kigeni. Ilikuwa? Mara, kulitokea tetemeko la ardhi lililozitikisa kuta hizo zikaanguka chini.

Kama maskini hao ndege wanalikuwa kule, wao pamoja na makinda wao wanalikuwa kama yule mwanamke, mume wake na watoto wake wachanga, huko Miami ama Okeechobee, wanalikufa pamoja na kule kuanguka kwa hizo kuta. Kama hao ng'ombe wanalisisimama karibu kujiegemeza kwenye hizo kuta, wanaliamia pamoja na hizo kuta. Hiyo imekuwa ni miaka mitatu iliyopita. Nina kipande cha gazeti hilo; la, Tommy Nickel analo sasa kwa ajili ya *Sauti* ya Wafanyabiashara Wakristo. Vichwa vya habari katika gazeti vinasema, "Ndege wanarudi makwao. Ng'ombe wanarudi kutoka kondeni."

¹⁴⁵ Kama Mungu, katika siku za Musa . . . siku za Nuhu, aliweza kuwaonya ng'ombe na ndege, waingie kwenye usalama, safinani, maangamizi yalikuwa yakija, dhoruba. Yeye angali ni Mungu yeye yule usiku wa leo, Yeye angali anawapenda ng'ombe na ndege. Na kama Yeye alifanya njia kwa ajili ya ndege na ng'ombe wapate kutoroka ile ghadhabu ya hukumu, ni zaidi sana vipi Yeye amefanya njia ya kutoroka kwa ajili yangu na yako wewe, ambao ni watoto wa uumbaji Wake! Ni zaidi sana vipi Yeye ameweka njia ya kuepukia kwa ajili yetu! Nasi tunamhisi Roho Mtakatifu akiivuta mioyo yetu. Saa inakuja. Tunaviona vivuli vya wa—wakati wa atomiki, tunaona vivuli vya wakati wa haidrojeni, tunaona mataifa yakivunjika, Israeli ikiamka.

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara walizotabiri manabii;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa
na hofu;
"Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu."

Hiyo ndiyo njia siku hizi! Nyote mnaujua ule wimbo wa kale wa Haywood.

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya watu inazimia kwa hofu;
Jazweni na Roho, taa zenu zitengenezwe na
ziwe safi,
Angalieni juu! Ukombozi wenu umekaribia.

¹⁴⁶ Dhoruba zinakuja. Kuna Mahali pa kujificha, loo, Mahali pa kujificha palipobarikiwa! Pako katika Kristo.

¹⁴⁷ Na tuimanishe vichwa vyetu kwa dakika moja. Ninawatakeni muwazie kwa uaminifu na kwa uchaji, kwa dakika nyingine moja.

¹⁴⁸ Umewahi kupata Mahali hapo palipobarikiwa pa kujificha, na ghadhabu? Kumbukeni, hakuna mahali pawili pa kujificha, kuna Pamoja tu. Huenda ukawa mfuasi mzuri wa kanisa fulani, ambalo sina ubaya wa kusema dhidi yake. Lakini kama hilo ndilo tu ulilo nalo, nayo maisha yako hayafanani na Kitabu cha Matendo, kama Roho Mtakatifu ambaye unashuhudia kwamba unaye hakufanyi uishi kama walivyoishi katika Kitabu cha Matendo, wala maisha yako yasingekiandika kitabu kingine,

afadhali usikie onyo. Kama mzabibu wa kwanza ulileta Kanisa la kipentekoste; mzabibu wa pili, ama tawi, hasa, kutoka kwenye huo Mzabibu, utaleta Kanisa lingine la kipentekoste, pamoja na ujuzi wa kipentekoste, likizaa matunda yale yale ambayo Kanisa la kwanza lilikuwa nayo. Je, unakaa kwenye Uwepo huo mtakatifu uliobarikiwa, wa Bwana? Umeipita kutoka mautini kuingia Uzimani? Unatulia juu ya mhemko fulani, baadhi ya matokeo ya kisaikolojia, ama hotuba fulani ya kiakili? Ama, wewe sikuzote unakaa katika Uwepo Wake, pamoja na tunda la Roho maishani mwako; uvumilivu, wema, upole, unyenyekevu? Je, unaweza kuvumilia mtu fulani kukusengenya, na, wewe unawapenda sana, hata moyoni mwako unawaombea? Ama, ni maskini ombi dogo la kichoyo, “Ee Bwana, ninajua ninapaswa kumwombea, lakini...” Loo, la, ndugu. Je, utamu huo na upendo wa Mungu, “Loo, pitia moyoni mwangu! Ee Roho Mtakatifu, pitia nafsini mwangu”? Kama hujapapata mahali hapo pa usalama, ndugu yangu!

¹⁴⁹ Nitafanya ziara yangu ya mwisho Phoenix, siku moja. Huenda hii ikawa ndiyo, yote nijuayo. Nao wakati wa mwisho Injili itakapohubiriwa kwenye mimbara hii, huenda huu ukawa ndio, mimi sijui. Tunaonekana kuwa karibu sana na wakati wa mwisho. Israeli imerudi kwenye nchi ya uenyeji wao, ile ishara ya mwisho iliyotolewa.

¹⁵⁰ Nilikuwa nikiangalia picha hivi majuzi usiku, ambamo wanawabeba wazee wao, vilema, kwenye meli na kadhalika, zinazolingia. Wakasema, “Kwani mmerudi nyumbani, mpate kufa?”

Kasema, “La, tumerudi ili kumwona Masihi.”

¹⁵¹ Msijali, mtini unachipusha majani yake, hiyo ndiyo ishara ya mwisho. Ile bendera, bendera ya kale kuliko zote ulimwenguni, inapepea juu ya Yerusalemu. Ni taifa linalojitegemea sasa, pamoja na jeshi lake lenyewe. Walipofushwa kwa kipindi kidogo, lakini wanarudi pamoja tena. Mungu aliahidi jambo hilo. Mwisho wa Mataifa utakuwa ni wakati huo. Wanamtazamia Masihi.

Mnajua, Mungu aliulizwa wakati mmoja, “Unaweza kuisahau Israeli?”

¹⁵² Kasema, “Anga zina urefu gani? Dunia ina kina kipi? Ipime!”

Nabii akasema, “Siwezi.”

¹⁵³ Akasema, “Wala nami siwezi kuisahau Israeli. Ni mboni ya jicho Langu.”

¹⁵⁴ Hiyo hapo ishara ya mwisho. Yesu alisema, “Mtakapoona mtini ukichipusha majani yake, jueni wakati umekaribia, hata mlangoni.” Israeli ikianza kurudishwa. Wana pesa zao wenyewe, yapata majuma manne yaliyopita. Lina pesa zake lenyewe, kila kitu. Ni taifa kamili.

Tunangojea nini? Kufungwa kwa Mataifa.

¹⁵⁵ Nayo ishara ya mwisho iliyotabiriwa kutolewa kwa Mataifa, imeonyeshwa kwa hili taifa na kote ulimwenguni, kama walivyofanya katika siku za Sodom.

¹⁵⁶ Wakati Yeye aliposema, “Yu wapi mkeo, Sara?” Mgeni, Yeye alijuaje alikuwa Sara? Naye alijuaje jina lake lilikuwa Sara, na ni mke wa Ibrahimu?

Kasema, “Yuko hemani nyuma yako.”

¹⁵⁷ Ndipo Sara akacheke moyoni mwake, huko nyuma hemani. Huyu Mtu akasema, “Kwa nini Sara akacheke?”

¹⁵⁸ Yesu alisema, “Haya yatakapotimia, wakati umekaribia.” Tumeliona tayari! Limepita. La pili ni hukumu.

¹⁵⁹ Wewe uko Mahali hapo pa kujificha palipobarikiwa, ewe rafiki? Mungu aturehemu! Endapo hupo, nawe ungetaka kukumbukwa usiku wa leo katika maombi, waweza kuinua mkono wako, useme, “Ndugu Branham, uniombee.” Mahali popote jengoni, inua... Mungu akubariki wewe, na wewe, wewe, wewe. Hilo ni jema. Mungu akubariki. Hilo ni... Mungu akubariki. Mtu mwingine yeyote aseme, “Nikumbuke, Ndugu Branham”? Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki wewe huko nyuma. Mungu akubariki huko nyuma kabisa, msichana. Mama huyu hapa, Mungu akubariki. Naam. Bwana akubariki, bwana; na wewe, pia. Loo, hilo ni zuri. Mtu mwingine, inua tu mkono wako.

Unasema, “Ndugu Branham, hilo linamaanisha nini?”

¹⁶⁰ Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki huko nyuma, bwana. Mungu akubariki hapa, mama. Hilo ni zuri sana.

¹⁶¹ “Inamaanisha nini, Ndugu Branham, ninapoinua mikono yangu?”

¹⁶² Unajua, kulingana na sayansi, huwezi kuinua mikono yako? Kama hakukuwa na uhai ndani yako, usingeweza kuiinua. Sayansi haijui uhai ni kitu gani. Wanajua ni uhai, bali hawajui ni nini. Hawawezi kuutengeneza. Basi ni kitu gani? Sayansi inasema ya kwamba, mikono yako, nguvu za uvutano zinaishikilia mikono yako chini, vile vile zinavyoishikilia miguu yako ardhini.

¹⁶³ Ila una roho ndani yako. Na, roho hiyo, kitu Fulani kimekuwa karibu nawe. Yesu alisema, “Hakuna mtu anayeweza kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu, kwanza, na wote alionipa Baba watakuja Kwangu.” Hivi huna furaha usiku wa leo kujua kwamba Mungu anaweza kuushughulikia moyo wako, ya kwamba kunayo Sauti ndogo pale, inayosema, “Njoo kwenye usalama”? Sasa angalieni, “Yeye ajaye Kwangu, sitamtupa nje kamwe.”

¹⁶⁴ Ilibidi kitu gani kitukie? Ilikubidi uwe na kitu Fulani kimekaa karibu nawe, kilichokwambia, “Umekosea.” Loo, unaweza ukawa ni mfuasi wa kanisa. Lakini, “Umekosea,” hujampokea Roho Mtakatifu, bado. Huko ndani ya Safina.

¹⁶⁵ Je, tunaingiaje ndani ya Safina? Si kutembea ndani Yake. Tunaingiaje ndani Yake? “Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja.” Waaminio wote wamebatizwa katika Mwili huo mmoja. Vipi? Kwa Roho Mtakatifu. “Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Sisi hapo, katika Mwili, salama.

¹⁶⁶ Kama sivyo, usimruhusu Shetani akudharau vya kutosha, usiku wa leo, kukuzuia kuinua mkono wako. Vema, hilo litafanya nini? Lilivunja kila kanuni ya kisayansi, ulipoinua mkono wako. Ilionyesha ya kwamba kitu fulani ndani yako kilikuwa kimefanya uamuzi. Kitu kikuu kuliko sayansi, kitu fulani kilichoasi kanuni za sayansi, kasema, “Ipo roho ndani yangu, inayosema, ‘Nimekosea.’ Na kuna Mmoja anayeketi karibu nami, na kusema, ‘Nikubali Mimi.’ Niliinua mkono wangu kuelekea mahali hiyo Sauti ilipotokea, Mbinguni. Unirehemu, Ee Mungu. Ninakuhitaji. Ninataka Roho Mtakatifu. Ninataka kuwa katika usalama. Ninazitaka dhambi zangu chini ya Damu. Nami nataka kutiwa muhuri katika Mwili wa Kristo, ili niweze kujisikia starehe, ninaweza kuifurahia miale ya uponyaji, ninaweza kufurahia miale ya uponyaji wa Kiungu nafsini mwangu, kuponywa kimwili mwilini mwangu, wa kutembea pamoja na Mwana-kondoo kila siku, salama. Haidhuru gazeti linasema nini, magazeti ya kila siku; nimesikia kutoka kwenye Gazeti kuu, linaloitwa Biblia. Nimeingia kwenye usalama. Haidhuru ni jambo gani linalotukia, mimi ningali salama. ‘Kwa kuwa wale,’ kama mauti yakinichukua, ‘wale walio katika Kristo, Mungu atawaleta pamoja Naye, kwenye Kuja Kwake.’ Ningali salama. Mauti hayawezi kunisumbua.”

¹⁶⁷ Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Mtu mwingine sasa kabla hatujaomba, “Nataka Mahali hapo salama pa kukaa, Ndugu Branham”? Kunaye mwingine ambaye hajainua mkono wao? Mungu akubariki, mama. Hilo ni zuri. Mungu akubariki huko nyuma upande wa nyuma. Hilo ni zuri sana.

¹⁶⁸ Sasa, Mungu yeye yule ambaye alikushawishi kwamba umekosea, yuko kukusahihishia hilo.

¹⁶⁹ Na tuviinamishe vichwa vyetu sasa, daima, na kuomba. Sema tu Naye sasa, katika njia yako mwenyewe. Ikiwa huwezi kufanya zaidi ya vile tu mtoza ushuru huyu aliyejipiga kifiani, kasema, “Mungu, unirehemu, mwenye dhambi.” Hivyo tu ndivyo ilivyompasa kusema; Mungu alijua hayo mengine. Basi akaenda nyumbani, amehesabiwa haki. Naomba uende vivyo hivyo, usiku wa leo, huru na dhoruba.

¹⁷⁰ Baba yetu wa Mbinguni, maneno haya machache yaliyochanganyikana na kutawanyika, kama tu nilivyojisia kuongozwa kuyasema, yalitolewa. Nami ninaomba ya kwamba, kwa njia fulani, kama yule mvulana mdogo aliyekuwa akizirudia alfabeti, akasema ndilo jambo pekee alilojua kufanya, “Wewe ulijua maneno yote, Nawe ungeweza kuziweka herufi hizo pamoja.” Uliuona urahisi wa moyo wake. Mungu, angalia chini juu ya maskini moyo wangu, usiku wa leo, na uone urahisi wa moyo wangu. Nao huu Ujumbe ulikusudiwa, Bwana, katika upendo na utamu, kwa ajili ya watu, kusudi wapate Raha hii ambayo umenipa mimi na maelfu ya wengine, ili waweze kumjua Yesu, Mwokozi pekee wa nafsi yao, ili aweze kuwaongoza kwa Baba yetu Mungu, na hapo wangekuwa na usalama uliochomekwa kifufu Mwake, kupitia ubavu Wake uliipasuliwa, na kumkubali Yeye, na kuwa huru na hukumu.

¹⁷¹ Na wengi usiku wa leo, Bwana, naam, wengi wameinua mikono yao. Ninaweza kufanya nini zaidi, Bwana, ila kuwaambia “kuamini”? Na kama waliamini, na walikuwa waaminifu katika hilo, haiwezekani kwao kutokuwa na Uzima wa Milele kwenye saa hii. Kwa kuwa, Wewe ulisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu.” Yalikuwa ni Yako; hayakuwekwa vizuri pamoja, labda, lakini Wewe unaweza kuyaweka pamoja. Na labda umefanya hivyo, kwa wale walioinua mikono yao, kwa kuwa Wewe ulisema, “Hakuna mtu awezaye kuja isipokuwa nimvute. Na wote wajao, sitamtupa nje, bali nitampa Uzima wa Milele, na kumfufua katika siku ya mwisho.” Tunajua, Bwana Mungu, kwamba ni Wewe! Waliinua mikono yao, wanakutaka Wewe. Sasa, Baba, ujaze moyo wao, ujaze moyo wao na wema na rehema, pamoja na Roho Mtakatifu. Jalia huu uwe usiku ambao kamwe hawatausahau, kwa sababu huu ndio ule usiku ambao walimpokea Yesu Kristo kama Mwokozi wao, na wakajazwa na Roho Mtakatifu.

¹⁷² Wakati tumeviinamisha vichwa vyetu. Kama unaamini ya kwamba Mungu husikia maombi yangu, nawe ungetaka nikuwekee mkono wangu na kuomba pamoja nawe, kama utanini tu... Wakati kila mtu wameinamisha vichwa vyao, na muziki kwa upole sana, tafadhalini. Ningetaka wengi wawezao, waje hapa, wanaotaka kukubali Ujumbe huu mkuu wa wokovu, Roho Mtakatifu. Na kusema “Ndugu Branham, ninataka kuja mbele sasa hivi, kukiri ya kwamba nimekuwa makosani. Lakini ninamtaka Roho Mtakatifu anisamehe, na kuwa mtamu kwangu sasa, na kunipa amani hapo wakati wa kutikiswa.”

¹⁷³ Mnajua, kila kitu kinachoweza kutikiswa, kitatikiswa sasa. “Lakini tunapokea Ufalme usioweza kutikiswa!” Huo ni Kristo.

¹⁷⁴ Waweza kuja na kusimama hapa madhabahuni, pamoja nami, uniache niushike mkono wako na kuomba pamoja nawe? Kama ukiweza, simama na uje sasa, wakati tukiimba kwa utulivu sasa. Ninyi mlionua mikono yenu, njoni hapa sasa na

kusimama madhabahuni, kwa dakika moja tu, kama ukitaka, tunapoimba kifungu hiki sasa.

Kuja nyumbani.

¹⁷⁵ Vipi kama huu ndio wakati wa mwisho utakapowahi kusikia Hili? Wazia hilo! Vipi kama ndio wakati wa mwisho? Vipi kama king'ora kitalia baada ya kitambo kidogo, huko mtaani, ni wewe, wanakuja kuuchukua mwili wako? Vipi kama, yapata saa nane usiku, umwite daktari wako, ni mshtuko wa moyo? Uko peke yako. Hili halitalia? Njoo sasa kwenye usalama, sivyo, kwa kuwa itakubidi kusimama kwenye siku za mwisho.

...Naja nyumbani.

Naja nyumbani, naja nyumbani,

¹⁷⁶ Mungu akubariki, Dada...?...[Ndugu Branham anaomba pamoja na watu madhabahuni, maneno yake mengi hayatambulikani—Mh.]...?...

Loo, kamwe...

¹⁷⁷ Hivi hutasimama tu, na kushuka pamoja na hawa wengine waliosimama pande zote madhabahuni? Njoo. Ni kuja hukumuni sasa. Hivi hutakuja? Njoo sasa, dhambi zako zimetubiwa sasa, haitakubidi kwenda hukumuni. Mungu awabariki watu hawa ambao ndio kwanza waje. Mungu akubariki, bwana. Hilo ni zuri. Mungu akubariki, msichana. Shuka uje huku. Njoo, bwana.

Nimetangatanga mbali...

Hima njoo, ndugu yangu Mhispaniola.

...mbali na Mungu,

Sasa naja...

¹⁷⁸ Hivi hutasimama sasa, na kushuka huku? Na tuombe. Njoo kwenye Kimbilio.

...ya dhambi kwa muda mrefu nimepitia,

Ee Bwana, naja nyumbani.

¹⁷⁹ Naomba niseme jambo hili, wakati kinanda kinaendelea kucheza. Ujumbe, usiku wa leo, ni Ujumbe wa upendo, neema, na onyo. Kesho usiku, Ujumbe huu huenda ukawa masikioni mwako mahali pengine, Ujumbe wa laana na hukumu. Wakati ukiwa na rehema ndani Yake, njoni muupokee. Sivyo, marafiki? Sina budi kukutana nanyi pamoja na Huu, yale niliyosema usiku wa leo, siku moja. Hivi hamtakuja? Acha uzungumze rehema, kwako. Wakati tukiimba mara nyingine tena, "Sasa Naja Nyumbani," hivi hutafanya hivyo?

¹⁸⁰ Kaa tu papa hapa, dada, mpendwa. Ninyi nyote kaeni papa hapa mkiweza, kidogo tu. Tunataka kufanya maombi pamoja na hawa madhabahuni. Acheni tu wakae papa hapa mahali walipo. Mara nyingine tena sasa.

Nimetangatanga mbali...

Simama, njoo. Sivyo? Ninakualika.

Sasa naja nyumbani;
Njia ya dhambi nimeipitia kwa muda mrefu
kupita kiasi,
Bwana, naja nyumbani.

Wakristo, ombeni sasa.

Naja nyumbani. . .

¹⁸¹ Njoo, ndugu yangu mwenye dhambi; njoo, dada; mlionunuliwa kwa Damu Yake, ambao Kristo aliwafia. Hutakuja sasa? Hebu nikushawishi, saa hii kuu, wakati hukumu inaning'inia mlangoni mwa taifa hili, milangoni mwa ulimwengu. Hutakuja? Ninakusihi, kwa niaba ya Kristo, njoo kwa Kristo wakati ukiweza! Acha iwe ni rehema, na si hukumu.

¹⁸² Sasa na tuuvumishe.

¹⁸³ Kunaweza kuwa na wengine, kidogo tu wakati tunapongojea hapa sasa? Watu mbalimbali wanachukua mahali pao kuwazunguka hao. Huu si ni wakati mzuri? Sijui, huenda ikawa ni mimi tu, bali ninajisikia tu vizuri sana sasa hivi. Hili ndilo ninalotamani, hili ndilo ninalopenda.

¹⁸⁴ Wakati nilipokuwa tu ni mvulana mhubiri, dada wa mhudumu mmoja aliniambia wakati mmoja, alitaka niende kwenye dansi pamoja naye. Nikamwambia sikwenda kwenye madansi. Akanionba nimpeleke kwenye sinema. Nisingefanya hivyo. Nikasema, "Siendi kwenye sinema."

Akasema, "Unapata wapi raha yoyote?" Nikasema, "Njoo pamoja nami mkutanoni."

¹⁸⁵ Usiku huo nilikuwa na mkutano wa hema. Nilikuwa tu mvulana, yapata umri wa miaka ishirini na mmoja, kijana mwanamume. Usiku huo, watu kadha walikuja madhabahuni. Nikamwona ameketi pale, akilia. Nikamwashiria, nikasema, "Uliniuliza swali jana usiku. Ninaweza kujibu usiku wa leo."

Kasema, "Lilikuwa ni lipi, Billy?"

¹⁸⁶ Nikasema, "Hii ndiyo furaha kuu kuliko zote ya wakati wangu." Kuwaona wenye dhambi wakija, kitu Fulani kinachoridhisha moyoni mwangu kinanena tu amani. Kuja nyumbani!

. . . naja nyumbani,
Kamwe. . .

¹⁸⁷ Napenda utamu tu. Unajisikia tu kama Roho Mtakatifu yupo, amefurahia, "umefanya vema, umefanya vema." Haya ni maandalizi ya ibada ya uponyaji, uponyaji wa kiroho kwanza. Mwili wa Kristo ni mgonjwa, unahitaji uponyaji, Mwili wa kiroho.

Naja nyumbani. . .

Sasa inamisheni vichwa vyenu. Kila mtu aombe. Kila mtu katika maombi.

. . . nyumbani,
Loo, kamwe nisitangatange tena.

¹⁸⁸ Sasa, afadhali umzingatie ndugu huyu hapa. Huna budi kuwa na kitu fulani humu ndani. Ninawataka wakae hapa kwa dakika chache zaidi.

. . . Mikono Yako (Ninyi kaeni papa hapa, hiyo
ni kweli.) ya upendo,
Mungu awabariki. 

60-0229 Dhoruba Ijayo
First Assembly Of God
Phoenix, Arizona Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org